



Na Rais  
Russell M. Nelson

# ZAWADI Kuu ya Mungu

Siku moja mimi na Dada Nelson tuliona samaki wa Skitropiki kwenye bwawa la samaki. Samaki wenye rangi za kung'aa na maumbo na ukubwa tofauti walienda mbele na nyuma. Nilimuuliza mfanyakazi aliyekuwa karibu, "Nani huwalisha samaki hawa wa kupendeza?"

Alijibu, "Mimi."

Kisha niliuliza, "Je, samaki wamewahi kukushukuru?"

Alijibu, "Bado!"

Baadhi ya watu ni kama samaki hao. Hawamtambui Mungu na wema Wake kwao. Ingekuwa vema kiasi gani ikiwa tungejua zaidi juu ya upendo wa Mungu na kudhihirisha shukrani Kwake.

## Shukrani kwa ajili ya Yesu Kristo.

Mungu alimtuma Mwana Wake, Yesu Kristo, kutusaidia. Alifanya hivyo kwa sababu anatupenda sana.

Yesu Alikuwa **kutukomboa**.

Kwa sababu ya **Upatanisho** Wake, tunaweza kufufuka baada ya kufa.

Kwa sababu ya Upatanisho Wake, tunaweza kurudi kuishi na Baba wa Mbinguni milele.

Yesu alielezea:

"Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima:

Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi: Naye kila aishiye na kuniamini hatakufa kabisa hata milele (Yohana 11:25–26).

Huu ndio ujumbe wa kupendeza wa Pasaka. ●

*Kutoka "Shukrani Ziwe kwa Mungu,"  
Liahona, Mei 2012, 77–80.*

